Mwongozo wa Jamii kwa Mkakati wa Usawa wa Kijinsia wa Mfuko wa Kimataifa

eannaso

Regional Platform
for Communication and Coordination
on HIV/AIDS, Tuberculosis and Malaria
For Anglophone Africa

Background:



Mfuko wa Kimataifa ni taasisi ya ufadhili. Inalenga kukuza jinsia kama nguzo ya kuzikabili Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria.

Mkakati wa Usawa wa Kijinsia wa Mfuko wa Kimataifa unahusisha Mkakati wa Usawa wa Kijinsia na Mkakati wa Utambuzi wa Mapenzi na Jinsia yaani Sexual Orientation and Gender Identities (SOGI). Hapa tunashughulikia Mkakati wa Usawa wa Kijinsia.

Mkakati wa Usawa wa Kijinsia wa Mfuko wa Kimataia unahusu usawa wa kijinsia katika kushughulikia Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria.

Mfuko wa Kimataifa unataka kuhakikisha kwamba misaada yake inasaidia usawa katika kuzuia, kutibu, huduma na usaidizi kwa wale wote wanaohitaji. Ilikufanikisha hili, ni wazi kwamba masuala ya usawa wa kijinsia kazima yashughulikiwe.

Kutokuwa na usawa kunasaidia kusambaza ugonjwa na kuathiri upatikanaji wa huduma za afya. Katika jamii nyingi, wanawake hawana haki sawa, fursa sawa na upatikanaji sawa wa huduma kama wanaume.

Mkakati wa Usawa wa Kijinsia unatizama jinzi Mfuko wa Kimataifa unaweza kuleta upendeleo chanya katika ufadhili katika mipango na shughuli ambazo zinashughulikia ukosefu wa usawa wa kijinsia na kuimarisha athari za maradhi kwa wanawake na wasichana.

Ukimwi, Kifua Kikuu na malaria unaathri wanawake, wasichana, wanaume na wavulana. Hata hivyo, tunaona ongozeko la athari kwa wanawake na wasichana ikifikia majanga haya matatu.

UKIMWI	KIFUA KIKUU	MALARIA
Katika nchi kusini mwa jangwa la Sahara, asilimia 75% ya watu waishio na Ukimwi kati ya 15 na 24 ni wanawake wadogo.	Katika nchi kusini mwa jangwa la Sahara, kutokana na janga la Ukimwi na Kifua Kikuu na kutokana na Ukimwi kuwa juu miongoni wa wanawake, kesi nyingi ya Kifua Kikuu kwa wanawake zinaripotiwa.	Nafai za kijinsia na masuala yanahusiana ya hili yanasababisha wanawake kuwa katika hatari zaidi ya wanaume ikifika kwenye athari za malaria na upatikanaji wa matibau.
Wanawake na wasichana wengi wanalazimika kuhudumia wanafamilia wagonjwa na watoto walioachwa yatima kutokana na Ukimwi	Katika nchi kusini mwa jangwa la Sahara, kesi nyingi za Kifua Kikuu zinaonyesha ni wanawake	Wanawake hususan wanawake wajawazito, wako katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa na kufa kutokana na malaria.
Wanawake na wasichana wanakumbwa na ubaguzi wa kiuchumi, kielimu, kisheria na kisiasa		Wanawake mara nyingi zaidi wanalazimika kuwahudumia wagonjwa wa familia.

Mfuko wa Kimataifa utasaidia maombi ya ufadhili ambayo itajumuisha mikakati ya afya ya umma ambayo inashughulikia ukosefu wa usawa katika jamii na kijinsia, pamoja na tabia ambazo zinachochea kuenea kwa magonjwa haya matatu.



Ili kufanya hivi, Mfuko wa Kimataifa unasisitiza masuala matau:

UIMARISHAJI WA MIFUMO YA KIAFYA

Taarifa nzuri zinaweza kusaidia kuonyesha haya majanga yanakaaje kulingana na mitazamo ya kijinsia na pia inaweza kuhakikisha kwamba mikakati mizuri ya kuyakabili yanafutwa

UIMARISHAJI WA MIFUMO YA KIJAMII

Mashirika ya Kijamii ni muhimu yasaidie katika kusimamia walw walioambukizwa na kuthuriwa na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria.

UFADHILI WA NJIA MBILI

Hii inatoa fursa kwa mashirika ya kiraia na mashirika ya kiafya ya jamii kupokea ufadhili

MFUKO WA KIMATAIFA UTASAIDIA NA KUFADHILI MAOMBI YA UFADHILI INAYO:

- Imarisha huduma na mikakati ya kukabili magonjwa ambayo inapunguza hatari zinahusiana na jinsia na athari za maambukizi
- Punguza mzigo wa maradhi kwa wale walio katika hatari kubwa zaidi
- Punguza athari za magonjwa haya matatu na;
- Shughulikia ukosefu wa usawa ambao ni wakimfumo na ubaguzi



MKAKATI UNA MALENGO MANNE ILI KUHAKIKISHA MISAADA YA MFUKO WA KIMATAIFA UNASHUGHULIKIA KUTOKUWA NA USAWA WA KIJIINSIA:

MIKAKATI MADHUBUTI

HII INAMAANISHA NINI?

NA SISI INATUHUSU NINI?

MIKAKATI MADHUBUTI	HII INAMAANISHA NINI?	NA SISI INATUHUSU NINI?
1. Kuhakikisha kwamba sera, mbinu na mifumo ya Mfuko wa Kimataifa inasaidia mipango ambayo inashughulikia ukosefu wa usawa wa kijinsia	1. Misingi ya usawa wa kijinsia unapaswa kuwa katika msingi wa maamuzi yote. Usawa wa Kijinsia ni sehemu muhimu katika mchakato mzima wa utoaji wa misaada.	Wakati wa kuandaa na kuwasilisha maombi ya ufadhili, Mifumo wa Kiuratibu ya Nchi (CCM) lazima ziweke suala la jinsia na pia kujumuisha mashirika ya kiraia. Kipaumbele utapewa katika Kujenga mtandao ambao unalenga mipango ambayo inakabili ukosefu wa usawa. Mfuko wa Kimataifa unaweza kutoa nyenzo za kwezesha kukuza mipango hii. Ushirikiano wa wadau lazima ujumuishe Kujenga uwezo ambao utazisaidia mashirika ya kinamama na mitandao ambayo itapokea ufadhili.
2. Kuanzisha na kuimarisha ushirikiano ambayo itassaidia maendeleo na utekelezaji wa mipango ambayo itashughulikia ukosefu wa usawa wa kijinisia na kupunguza athari kwa wanawake na wasichana, kutoa usaidizi wa kitaalam, na Kujenga uwezo wa makundi ambayo kwa sasa hayashiriki katika michakato ya Mfuko wa Kimataifa ila yangepaswa kushiriki.	2. Washirika wanapata msaada katika kuhakikisha usawa wa kijinsia ni sehemu ya ufadhili wa Mfuko waKimataifa.	
3. Kuandaa mkakati madhubuti wa mawasiliano na uenezi ambao unakuza mkakati wa Usawa wa Kijinsia na kuima-risha mipango kwa wanawake na wasichana pamoja na wanaume na wavulana.	3. Kuhakikisha jkila mtu anapata taarifa zote zinazohusu usawa wa kijinsia	
4. Kutoa uongozi, ndani nan je kwa kusaidia, kueneza na kuipa sauti Mkakati wa Usawa wa Kijinsia.	4. Kuhakikisha wale waliopo katika Mfuko wa Kimataifa wana uwezo na ujuzi wa kukabili ukosefu wa usawa wa kijinsia	

WASILIANA NA MPANGO WA KIKANDA

Regional Platform for Communication and Coordination for Anglophone Africa Hosted by EANNASOArusha, TanzaniaTel: +255 737 210598Email: eannaso@eannaso.org | Website: www.eannaso.org
Facebook: www.facebook.com/eannaso.org | Twitter: @eannaso